# WIZARA YA MAJI

## MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA JIJINI DODOMA

## (DUWASA)

**TAARIFA YA MAENDELEO YA UTEKELEZWAJI WA MRADI WA MAJISAFI WA NTOMOKO, KATIKA WILAYA YA KONDOA.**

**(Taarifa kwa Katibu Mkuu)**

Imeandaliwa na:

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA)

S.L.P 431,

**DODOMA**

**TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI JUU YA MRADI WA MAJI WA NTOMOKO KWA KATIBU MKUU**

Ndugu Mgeni Rasmi Napenda kuchukua nafasi hii, kuwakaribisha wageni waalikwa wote hapa Kondoa kushuhudia uwekwaji wa saini kwenye mradi huu wa maji wa Ntomoko.

**Ndugu Mgeni Rasmi**

**Utangulizi**

Mradi wa maji wa Ntomoko ulibuniwa mwaka 1971 na kuanza kujengwa mwaka huo na ulikamilika mwaka 1973. Ulibuniwa kwa ajili ya kutoa huduma ya maji kwenye vijiji 17. Vijiji hivyo ni Makirinya, Kirere cha Ng'ombe, Kinkima, Churuku, Mtakuja, Hamai, Songolo, Chandama, Mapango, Itolwa, Mlongia, Goima, Igunga, Jenjeluse, Jinjo, Lusangi na Jangalo. Katika jitihada za kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji kwenye vijiji vya mradi wa Ntomoko, bwawa la Mwisanga lilijengwa katika miaka ya 1978.

Kutokana na bwawa hilo kujaa tope jingi (silting) lililosababisha kiasi cha maji kwenye bwawa hilo kuwa kidogo, bwawa halikuweza kuhudumia maeneo yaliyokuwa yamelengwa ya vijiji 17 vya mradi wa Ntomoko. Kujaa tope kwenye bwawa hilo kulisababishwa nakuongezeka kwa wakazi pamoja nashughuli za kijamii na kiuchumi zilizo kuwa zinaendelea kufanyika kwenye bonde la mkondo wa maji uliokuwa unaingiza maji kwenye bwawa hilo, Aidha, ilionekana kuwa kuna umuhimu wa kujenga chujio la kuchuja tope ambalo lilikuwemo kwenye maji.

Wakati ujenzi ukiendelea ilionekana kuwa kadri muda ulivyokuwa ukipita tope lilikuwa likiongezeka kwa kasi kwenye maji ya bwawa na hata kwenye bwawa lenyewe. Pamoja na kuongezeka kwa tope kwenye maji, iliamuliwa kuwa maji ya bwawa hilo pamoja na kuwa na tope jingi yaanze kutumika kwa kupitishwa kwenye mabomba yaliyofungwa ili kuhudumia watu kwenye vijiji vilivyolengwa.

Matokeo yake ni kuwa tope lilikwama kwenye mabomba, maji kushindwa kupita na mabomba mengi kufumuka na kusababisha ukosefu wa huduma ya maji kwa walengwa. Kutokana na tathmini iliyofanyika, kwa kuzingatia wingi wa maji kwenye chanzo cha maji ya mtiririko cha Ntomoko pamoja na mabomba yanayochukua maji kutoka kwenye chanzo hicho, mradi una uwezo wa kuhudumia watu wapatao 23,400 ambao kwa sasa wameongezeka mara tatu ya ilivyokuwa hapo mwanzo.

Kulingana na kipenyo cha mabomba na uchakavu wake hivi sasa, ni vigumu kwa maji kufika kwenye vijiji vingine vilivyopo mbali kutoka kwenye chanzo cha maji.

**Ndugu Mgeni Rasmi**

**Hali ya Mfumo wa Maji Katika Eneo la Mradi wa Ntomoko**

Hali ya mfumo wa maji imekuwa siyo ya kuridhisha na kuweza kukidhi mahitaji ya maji kutokana na ongezeko la wakazi wa maeneo hayo kutoka watu 23,400 mwaka 1973 na kufikia takribani watu 75,800 mwaka 2018 (kutokana na sense ya mwaka 2012). Aidha, hakuna maji yakutosha yakupeleka kwenye vijiji 9 vya ukanda wa chini bila ya kuvifungia vile vijiji 8 ambavyo viko karibu kabisa na chanzo.

Mahitaji ya maji kwa vijiji 8 vya ukanda wa juu pia yameongezeka na kusababisha huduma ya maji kutolewa kwa mgao kwenye vijiji hivyo 8 vya Makirinya, Kirere cha Ng'ombe, Churuku, Mtakuja, Kinkima, Igunga, Jinjo na Lusangi. Vijiji 9 vilivyobaki vya Hamai, Songolo, Chandama, Mapango, Itolwa, Mlongia, Goima, Jenjeluse na Jangalo vilivyoko ukanda wa chini havipati maji kabisa.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Kumekuwa na jitihada mbalimbali za kufanya ukarabati wa mradi huu ili kuweza kutoa huduma ya maji kwa Wananchi. Hata hivyo, katika kipindi chote cha ukarabati wa mradi huu, kumekuwa kukijitokeza changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na mabomba kupasuka, maji kutotoka kwenye vituo, hivyo kusababisha mradi kutokidhi malengo yaliyo kusudiwa.

Mnamo tarehe 04/05/2018 Wizara ya Maji na Umwagiliaji iliiandikia DUWASA barua ikielekeza kuchukua hatua za haraka ya kuandaa gharama zinazohitajika kukarabati mradi wa Ntomoko na kusimamia kazi ya ukarabati wa mradi huo.

DUWASA kwa kushirikiana na Wahandisi wa Maji wa Wilaya za Kondoa na Chemba wamefanya usanifu wa mradi huu na kuanza taratibu za manunuzi ya Mkandarasi wa Ujenzi. Mradi huu utatekelezwa na kampuni ya CHINA RAILWAY SEVENTH GROUP COMPANY LIMITED chini ya usimamizi wa DUWASA pamoja na Wahandisi wa Maji wa Wilaya za Kondoa na Chemba.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Mradi huu wa maji utagharimu jumla ya Shilingi Bilioni 2. 269 za kitanzania ambao utawezesha maji kufika katika matenki ya Makirinya yenye lita 45,000, Kinkima lenye lita 90,000 na Lusangi lenye lita 90,000. Hivyo, mradi huu utaweza kuhudumia vijiji vya Ntomoko (Fai), Makirinya, Kinkima na Lusangi.

**Ndugu Mgeni Rasmi,**

Utekelezaji wa mradi huu utaanza tarehe 18/02/2019 yaani wiki moja baada ya kusainiwa kwa mkataba huu leo na utatekelezwa kwa miezi 12, hivyo utakamilika mwezi Februari, 2020.

Ndugu Mgeni Rasmi Mradi huu utahusisha kazi zifuatazo; Ununuzi wa mabomba ya chuma (Ductile Ironna GS) yatakayotumika kukarabati maeneo yenye uchakavu kwa jumla ya umbali wa mita 8,000 yenye vipenyo vya 200mm (Urefu wa mita 5,000), 150mm (urefu wa mita 1,200) na 50mm (urefu wa 1,800m). Kuchimba na kulaza mabomba pamoja na viungio vyake. Kuweka air valves na washouts kwenye mtandao wa mabomba. Kujengea mabomba kwa zege (anchor blocks) ilikuyashikilia sehemu korofi (zenye mito, mifereji ya maji).

Kununua na kuweka pampu itakayo tumia Nishati ya jua kuhudumia Ntomoko (kitongoji cha Fai) Kukarabati matenki ya Makirinya (lita 45,000), Kinkima (lita 90,000) na Lusangi (lita 90,000). Kujenga chemba mpya kwenye maeneo yatakayoongezewa valves na kukarabati zile za zamani.

Ndugu Mgeni Rasmi Fedha za kutekeleza mradi huu ambao mkataba wake tunausaini leo, zinatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Maji.

Ndugu Mgeni Rasmi Aidha, vijiji vingine vilivyobaki vya Mtakuja, Igunga, Goima, Songolo, Jinjo, Jangalo, Mlongia, Jenjeluse, Chandama, Itolwa, na Mapango, Serikali imetenga fedha kupitia ufadhiliwa India kwa ajili ya kujenga mabwawa katika eneo la Chemba na hivyo kuwapatia maji wananchi wa vijiji hivyo. Mradi huo unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2020/2021.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**